



## TANGAZO KWA UMMA

(No. GA.128/192/01/C/42)

### MWONGOZO KUFUATIA CHANGAMOTO KWA WATUMIAJI WA MFUMO WA TANePS KATIKA KIPINDI CHA TAREHE 17-18 MACHI 2022

1. Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuwataarifu Wadau kwamba imekuwa ikipokea maombi ya msaada kuhusu Mfumo wa TANePS kufuatia changamoto yao ya kushindwa kufungua au kuwasilisha Zabuni kupitia Mfumo wa TANePS katika kipindi cha tarehe 17-18 Machi, 2022. Baada ya kufanya uchunguzi, changamoto hiyo ilitatuliwa, lakini baadhi ya Zabuni ziliathirika na hivyo kushindwa kuendelea katika Mfumo.
2. Hivyo basi, kutokana na changamoto hiyo, Mamlaka inatoa mwongozo ufuatao kwa Taasisi Nunuzi :-
  - i) Zabuni zote zilizoathirika na ambazo zilikuwa zinatumia njia ya "**Mini-competition**" kwa ununuzi wa bidhaa na huduma mtambuka, "**Minor value Procurement**"; na "**Single Source Tendering/Selection**", inaelekezwa zitangazwe upya kwenye mfumo wa TANePS;
  - ii) Zabuni zote zilizoathirika na ambazo zilikuwa zinatumia utaratibu wa **Mwaliko** ("**International/National Shopping**"; na "**International / National Restricted Tendering /Selection**") inaelekezwa zitangazwe upya kwenye Mfumo kwa nusu ya muda wa kawaida, kwa mujibu wa **Jedwali la Nane la Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013**, kama zilivyorekebisha; na
  - iii) Zabuni zote zilizoathirika na ambazo haziko katika kundi la (i) na (ii) hapo juu, zitashughulikiwa kila moja kutokana na hali yake; na taarifa za Zabuni hizo zitumwe kupitia barua pepe ya [helpdesk@ppra.go.tz](mailto:helpdesk@ppra.go.tz).
3. Wazabuni wanashauriwa kufuatilia fursa za zabuni katika Mfumo ili waweze kushiriki katika michakato kwa zabuni zitakazotangazwa upya, kama iliyovyoelekezwa hapo juu.
4. Mamlaka inaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Imetolewa tarehe 21 Machi, 2022, na

Dkt. Irene C. Isaka  
**AFISA MTENDAJI MKUU**